

# Kifo mbona?

Kifo ninakuchukia, waiba bila huruma,  
Kifo tunakulilia, mbona watupa gharama?  
Kifo mbona watishia, maisha yetu wandama,  
Kifo mbona tuibia, mebaki kushika tama.

Kifo wewe una wivu, kiona mafanikio,  
Kifo wewe si mvivu, machoni na masikio,  
Kifo wewe huna livu, milele sikitikio,  
Kifo mbona kutuibia, mebaki kushika tama.

Kifo njiani hujali, unachukua kokote,  
Kifo iba kwa ajali, huna huruma kwa wote,  
Kifo usiku hulali, unatafuta popote,  
Kifo mbona tuibia, mebaki kushika tama.

Kifo mbona situlie, hiana bila rehema,  
Kifo mbona sisikie, wataka iba daima!  
Kifo utuhurumie, maisha haya matama,  
Kifo mbona tuibia, mebaki kushika tama.

*Josphat Cheruiyot  
Chuo cha Seku, Kitui*